# Jarida la UQAB

Toleo 11
Disemba 2017 Miladi
Rabi-ul-awwal 1439
Hijriya



**Serikali za Kirasilimali Zinaendeshwa kwa Manufaa na sio Huduma bora**


**Ukabila Ni Uvundo Unaoendeleza Ukoloni Wa Kisiasa**

**Matumizi Mabaya ya Teknolojia ya Mawasiliano**

**Kashfa ya Ngono ya Westminister**

**Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi -Halaqa 7**

**SWALI / JAWABU: Matokeo ya Kisiasa Katika Mkoa wa Catalonia!**

## Siasa za Chuki na Migawanyiko ni Dalili Tosha ya Kufilisika Kifikra kwa Siasa ya Demokrasia na Wafuasi Wake

Offisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

KUMB: 02 / 1439 Hijria | Ijumanne, 10 Rabiul-Awwal 1439 Hijria | 28/11/2017 Miladi


# Siasa za Chuki na Migawanyiko ni Dalili Tosha ya Kufilisika Kifikra kwa Siasa ya Demokrasia na Wafuasi Wake

**Taarifa kwa Vyombo vya Habari**

Hatimaye, rais Uhuru Kenyatta ameapishwa kuhudumu kwa muhula wa pili kwenye sherehe iliohudhuriwa na viongozi wa mataifa mbalimbali na kususiwa na wanasiasa wa upinzani. Hafla hii imekuja huku nchi ikighubikwa na migawanyiko ya kikabila, semi za chuki na umwagikaji wa damu. Kwenye hotuba yake rais Kenyatta amekiri kuwa anakabiliwa hapo mbeleni na kazi ngumu ya kuleta uwiano na kuunganisha taifa lililogawanyika na ambalo hujipata kwenye shimo la taharuki kila wakati wa uchaguzi.

**Sisi Hizb ut Tahrir Kenya tungependa kusema yafuatayo:**

Matatatizo ya migawanyiko ya kikabila, taharuki na mauaji yanayoshuhudiwa katika misimu ya uchaguzi hayo yote yanafichua kufilisika kifikra kwa wanasiasa wa Kidemokrasia kiasi cha kuwa kampeni zao hujikita katika kuibua chuki na mitafaruku baina ya raia. Na hili sio kwa wanasiasa wa Kenya bali hata kwa mataifa ya magharibi kama tunavyoona kampeni ya chaguzi zao jinsi wanavyochochea chuki kati ya Waislamu na Wakristo, baina ya watu weupe na weusi. Yote haya ni dalili wazi sasa wanakubali kuwa hawawezi kushinda kura kwa kuegemea sera zao mbovu za kisiasa, kiuchumi na kijamii. Isitoshe ni kuthibitisha kutojimudu kwa mfumo katika kuondoa matatizo ya migawanyiko ya kikabila.

Ni kweli kuwa matatizo ya Kenya yanahitaji kutatutiliwa lakini kwa kuwa wanasiasa wa mirengo yote ima walioko katika utawala au upinzani wote wamekumbatia sera mbovu za mfumo wa kibepari wa Kirasilimali ambao ndio chanzo halisi cha matatizo yote yanayoikumba Kenya na ulimwengu kwa ujumla. Mfumo wa kibepari umejengwa juu ya kumtajirisha tajiri kwa kumnyonya mlalahoi hatimaye kukuza mwanya mkubwa baina ya mabwenyenye na walalahoi. Na hii ndiyo sababu iliopelekea serikali tatu zilizotawala Kenya kushindwa kutatua matatizo ya raia licha ya kufanyika marekebisho kadhaa ikiwemo kubadilishwa kwa katiba na kamati za uchaguzi. Hivyo matakwa ya upinzani kutaka merekebisho ya mfumo wa uchaguzi, kuheshimu utawala wa sheria yote hayo ni kujaribu kupaka rangi mfumo ulio na msingi muovu.

Tunasema Kenya na ulimwengu jumla inahitaji Uislamu ulio na muundo mzuri wa Kisiasa (Khilafah) utakao kuwa na suluhisho kwa matatizo ya wanadamu wote. Uislamu hufasiri siasa kuwa ni kusimamia kwa dhati mambo ya watu wala sio ung'ang'anizi wa utawala baina ya wanasiasa kufikia manufaa yao ya kibinafsi. Nidhamu ambayo vyama vya kisiasa ndani yake vitakua sio vyombo vya kufikia tu madaraka bali kuihesabu serikali ili iweze kutimiza majukumu yake kwa raia kikamilifu.


**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari**
**Hizb ut-Tahrir Kenya**

# Serikali za Kirasilimali Zinaendeshwa kwa Manufaa na Sio Huduma Bora Kiasi Kwamba Miradi Inabuniwa kuwa kama Ng'ombe Mwenye Kukamuliwa Pesa




**Habari:**

Wizara ya Hazina imeikanusha kampuni iliyopewa mkataba kukusanya mapato kwa niaba yake kutoka kwa watumizi wa mtandao wa eCitizen, hili likizidisha usiri wa namna gani kampuni ya kibinafsi ilichukua jukumu ambalo kiasili linasimamiwa na Mamlaka ya Ukusanyaji Ushuru (KRA). [Business Daily]

**Maoni**

Kabla hata vumbi halijatulia kutokana na sherehe za mamilioni ya Wakenya waliocheza kwa furaha na kupata afueni baada ya serikali kuanzisha Mpango wa Dijitali. Mpango huo ambao Waziri wa Hazina, Henry Rotich alisema kuwa utadhibiti ufisadi na kuziba mianya inayopelekea ufujaji wa mali ya umma katika serikali ya kitaifa na za kaunti; na mpango huo ukatengewa bilioni Ksh1.9 ili utekelezwe. Sehemu ya mpango huo ulipelekea kuzinduliwa kwa Huduma Kenya, mtandao wa eCitizen, Huduma ya Vijana kwaTaifa (NYS) na Nidhamu ya Udhibiti wa Habari za Matumizi ya Fedha (IFMIS) ambayo ilitarajiwa kusimamia ununuzi na ulipaji kidijitali, yote hayo yakifanyika kati ya Novemba 2013 na 2014.

Walichokuwa hawakijui Wakenya ni kuwa uzinduzi huo ulikuwa ni miradi ya 'ngo'mbe pesa' ikiwa na lengo la kuwaibia mabilioni kutoka katika uchumi wao ambao tayari unaendeshwa kwa madeni makubwa na huku wakitozwa ushuru kutoka kila kona ya mifuko yao! Kashfa nyingi ziliibuka kutokana na mpango huo tukitaja baadhi tu:

1. Gharama ya kuweka afisi ya Vituo vya Huduma ilikuwa chini ya uchunguzi wa Kamati ya Uhasibu wa Fedha za Umma (PAC) ambapo mamilioni yalipotea kutokana na kuongeza bei za vitu na ununuzi wa huduma. Mfano rekodi zaonyesha kuweka afisi kuligharimu milioni Ksh437 kutoka kwa bilioni Ksh1.2 zilizotumiwa na kitengo cha usimamizi wa huduma kwa umma katika mgao wa fedha za 2013/2014. Miongoni mwa gharama za vituo vya Huduma ilikuwa Ksh174,000 zilizotumika kununua kalamu 20 za

Endelea Uk..4

wino! Pia kulikuwa na ununuzi wa vibeba habari (4GB Flash Disks) 100 kwa gharama ya Ksh242,500. Katika hali nyingine, gharama za vituo vya Huduma kwa shauku zilikuwa sawia: milioni Ksh2.4 za uchapishaji posta kidijitali, milioni Ksh1.2 za habari, milioni Ksh2.4 za kuhariri na nusu ya hiyo kwa bango. Baadhi ya biashara hazikueleweka, kama ulipaji wa "ununuzi wa vitu ndani ya Vituo vya Huduma" ambapo Ksh282,534 zilitumika. Kwa shauku, Wizara ilitumia milioni Ksh10.6 ili kukarabati afisi za Kamishna wa Mkoa wa Nyeri na kuifanya kituo cha Huduma, pesa ambazo zilitosha kujenga jengo jipya.

2. IFMIS iliharibiwa kiasi kwamba tukashuhudia kashfa ya NYS ambayo zaidi ya bilioni Ksh1.8 ziliibiwa, bilioni Ksh5 zikikosa uhakiki katika Wizara ya Afya na orodha inaendelea.

3. **Kashfa mpya ikiwa ni ya mtandao wa eCitizen** ambapo zaidi ya bilioni Ksh5.6 'hazijulikani' aliyekuwa akizichukua tokea mwaka 2014 ambapo ulizinduliwa. eCitizen ni mtandao wa kidijitali ambao serikali ya Kenya inatoa huduma msingi kama usajili wa pasipoti, cheti cha uendeshaji gari, usajili wa vyeti vya biashara, veyti vya gari na hatimiliki za ardhi. Kila huduma katika mtandao huo inagharimu Ksh50 inayotozwa kama 'ada ya urahisishaji' zaidi ya gharama ya kawaida. Hii ikiwa ni ongezeko juu ya gharama zinazotozwa na kampuni za pesa simuni wakati wa kulipia. Mfano, mtu anataka kukifanya upya cheti chake cha uendeshaji gari kwa mwaka angelitakiwa kulipa Ksh600. Lakini chini ya mtandao huo wa Serikali, gharama hiyo inakuwa Ksh650 kando na ada ya kulipia simuni.

Wahusika katika kashfa hiyo ni Wizara ya Hazina na Webmasters – ambao walitengeza huo mtandao, Safaricom – ambao waliupa mtandao huo Nambari ya Ulipiaji ya 206206 na Goldrock Capital ndio wakusanyaji pesa hizo ambazo ni mjumuisho wa Ksh50 za 'ada ya urahisishaji' tangu mwaka 2014! Imekuwa wapi Mamlaka ya Ukusanyaji Ushuru (KRA) maanake wao ndio shirika msingi lililoidhinishwa na sheria kukusanya mapato kwa niaba ya serikali?! Lakushangaza kila mmoja wa wahusika anazusha vurugu tangu kashfa hiyo ifichuke na hakuna hata mmoja aliye tayari kubeba lawama!

Kinachofanyika Kenya kuhusiana na kashfa za ufisadi kufuatana moja baada ya nyingine kila mwaka si tu katika sekta ya umma bali hata katika sekta ya kibinafsi ufisadi upo katika viwango vya juu na hakuna wa kuihesabu sekta ya kibinafsi ambayo ni 'mchungaji' wa sekta ya umma! Ni natija ya utekelezwaji wa mfumo batili wa urasilimali ambao aqeedah yake ni ilmaniy – kutenganisha dini na serikali/maisha. Hivyo basi inapeana demokrasia kupitia wanasiasa wa kidemokrasia ukiritimba katika kudhibiti/kutunga sheria za mambo ya kimaisha kwa msingi wa akili zao finyu na kwa kipimo makhsusi cha vitendo kilicho jengwa juu ya manufaa/maslahi. Hivyo basi, sheria zote au miradi yote inayotokamana au iliyopitishwa na matajiri warasilimali wanaojumuisha wanasiasa wa kidemokrasia; si tu kuwa haina msukumo wa huduma bora bali pia imelenga kunyonya na kuiba mali za umma ili kushibisha hamu yao ya anasa za ulimwengu ambazo ni za muda mfupi na zenye kutia majaribu mno. Kwa kuwa hakuna kuhesabiana kutokana na kuwa wote mtungaji sheria na mtendaji wote ni sehemu ya 'klabu ya walio na haki zaidi, ambao wako juu ya sheria!

Allah (swt) asema:

وَمَا الْحَيَاةُ الدُّنْيَا إِلَّا لَعِبٌ وَلَهْوٌ ۖ وَلَلدَّارُ الْآخِرَةُ خَيْرٌ لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ ۗ أَفَلَا تَعْقِلُونَ

**Na maisha ya dunia si chochote ila ni mchezo na pumbao tu. Na hakika nyumba ya akhera ni bora zaidi kwa wanao mcha Mungu. Basi, je, hamtii akilini?** (Al-An'aam: 32)


Mtume (saw) naye pia akafafanua thamani ya maisha haya ukilinganisha na akhera. Akasema: **Maisha haya ya dunia ulinganisha na ya akhera ni kama mtu kutia kidole chake ndani ya bahari na kisha akakitoa na kulinganisha na maji yaliyobakia katika kidole chake na maji yaliyobakia baharini** [Sahîh Muslim (2858)]

Ni ndani ya Uislamu pekee ambapo mtu anabeba majukumu ya uongozi kwa dhumuni moja pekee nalo ni kutoa huduma bora kwa msukumo wa kutafuta radhi za Mola wake (swt) huku akiwa na matarajio ya kuingizwa peponi. Ndani ya mtu huyo uchajimungu umemakinika na hakuna kitakacho mkwaza asifikie shabaha yake ya kubuni na kupanga miradi ambayo imo ndani ya mipaka ya Uislamu na ambayo itaboresha maisha ya wenzake chini ya kivuli cha Serikali ya Kiislamu iliyo simamishwa kwa Njia ya Utume.

**Ali Nassoro**
**Mwanachama wa**
**Hizb ut Tahrir Kenya**

1. http://www.businessdailyafrica.com/news/Treasury-now-disowns-eCitizen-platform-company/539546-4185702-15ly2cq/index.html
2. http://www.businessdailyafrica.com/corporate/Kenyans-pay-more-for-State-services-on-eCitizen-portal/539550-3389922-sgqfg0/index.html
3. http://www.businessdailyafrica.com/economy/Big-bet-on-E-payments-to-seal-fraud-loopholes--/3946234-2748762-bnjk55/index.html
4. http://www.nation.co.ke/news/Huduma-costs-set-to-be-scrutinised/1056-2944766-h4oa57z/index.html
5. http://www.nation.co.ke/news/1056-3466304-5fes0sz/index.html

# Ukabila Ni Uvundo Unaoendeleza Ukoloni Wa Kisiasa




Katika maradhi sugu yanayosumbua Kenya ni ukabila. Uvundo huu hutoa harufu mbaya zaidi wakati wa uchaguzi kama chaguzi mbili zilizokuweko yapata miezi michache iliyopita. Vinara wawili wa kisiasa Uhuru Kenyatta na Raila Odinga wakaonekana wakijumuisha kabila moja hadi jengine kujaribu kuhifadhi na kupigania malengo yao ya kisiasa.

Ukabila ni katika mafungamano duni yasofaa kuwaunganisha jamii na hufasiriwa kama kujifakhirisha mbele ya kabila jengine na kushikilia kuwa kabila lako linastahiki kupewa hadhi kubwa kuliko makabila mengine. Fungamano hili hutokamana na hisia za kibinadamu za kuhifadhi maisha ambayo ni sehemu ya maumbile ya mwanadamu nayo humpelekea mwanadamu kufukuzia ubwana ndani ya kabila lake kisha akiupata husonga mbele kutaka kutawala kabila jengine. Sifa ya ukabili ni kuwa huchochea pakubwa uhasama ndani ya jamii ya wanadamu juu ya kufikia ubwana huo.

**Kwanza: historia ya siasa za kikabila na athari yake kwa Kenya**

Baada ya walowezi wa kizungu kukoloni Kenya kwa miongo kadhaa ambapo walichezea hisia za makabila ya Kenya na kama turufu ya kisiasa kuendeleza ukoloni wao. Na hata baada ya wakoloni kujifanya wanatoka Kenya kwa madai kuipa uhuru, tayari walikuwa wamehakikisha kwamba mbegu za ukabila zimeanza kuota ambapo mawakala wake wa kisiasa walitakikana kupalilia mimea ya jinamizi la ukabila. Miaka ya sitini kulianza kile wachambuzi wa kisiasa nchini Kenya wanakiita nadharia ya 'Usaliti wa WaLuo' kwa maana kuwa wakikuyu ndio wanaowasaliti wajaluo. Utawala wa Kenyatta baba na wale waliojulikana kama 'Kiambu Mafia' ulihusika pakubwa katika utekaji nyara na uuaji wa kisiasa dhidi ya wanasiasa wa eneo la Nyanza. Mauaji ya Thomas Joseph Mboya Julai 5 1969, kuzuiliwa korokoroni kwa Jaramogi Oginga Odinga na matukio mengine hutajwa kama mambo yaliyotia chachu zaidi chuki za kikabila baina ya wajaluo na Wakikuyu. Kwa upande wa Wakikuyu, nao wana nadharia inayojulikana kama 'Nadharia ya WaKikuyu' inayosema kwamba WaLuo hawathamini usalama na utulivu wa taifa. Kisa cha Hospitali

*Endelea Uk..6*

ya Russia ambao msafara wa rais Jomo Kenyatta ulishambuliwa na vijana wa Kijaluo kwenye sherehe za ufunguzi wa Hospitali hiyo iliojengwa na serikali ya Urusi kwa thamani ya pauni milioni 1.2. Tukio hili lilitokea miezi michache tu baada ya mauaji ya Tom Mboya ambao watu wengi waliuwawa. Kisa hiki kilikuja kujulikana kama 'Kisumu Massacre'.

**Pili: athari ya ukabila**

Ukiachilia mbali uhalisia huu, kumeripotiwa visa vya ukabila katika sekta nyingi nchini Kenya. Kuanzia utawala, usalama, afya, na uchumi na biashara. Hali imekuwa kabila zinazoungana na kuunda utawala hupata mgao mkubwa dhidi ya kabila za kiupinzani. Tume ya Uwiano na utengamano ya Kitaifa (NCIC) mwaka jana (2016) ilifanya ukaguzi wa mjumuisho wa makabila katika huduma ya umma za kaunti katika mashirika ya serikali yapatayo 185 na kubaini kuwa kati ya majimbo 47 ni kumi na tano pekee ndio kwa asimilia thelathini yameajiri kabila za maeneo ya nje ya kaunti hizo. Ikakuta kuwa majimbo yaliosalia yaani 32 huajiri watu wa kabila linalopatikana eneo hilo kwa asilimia 70.

Siasa za Kenya ni zenye kuzunguka kwenye mkondo wa kikabila. Tokea uhuru wa bendera, vita na miungano ya kikabila ilianza lakini chini ya vazi la vyama viwili vikuu; Kenya Africa National Union (KANU) na Kenya African Democratic Union (KADU). Chama cha KANU asili kilikuwa na muungano baina ya makabila makuu pinzani; Wakikuyu na Wajaluo. KADU nayo ilikuwa ikiunganisha makabila mengine yaliyo kabiliwa na unyanyasaji. Kinaya ni kuwa utawala wa Kenyatta ulimfanya Moi kuwa mwandani wake aliye tayarishwa kuchukua hatamu za uongozi baada ya kufanywa makamu wa rais kuanzia mwaka 1966 hadi 1978. Jambo hili halikupokelewa vyema na Jaramogi Oginga Odinga. Utawala wa Moi ulikuwa maarufu kwa kuendeleza siasa ya kugawanya watu utawale (Divide and Rule politics). Matokeo yake kukalipuka vita vikali vya kikabila 1992 baina ya Kalenjin na Wakikuyu ambao inakisiwa zaidi ya watu elfu tano [5,0000] waliuwawa. Mwaka wa 2007 Kenya ikalipuka tena kwenye mlipuko wa vita vya kikabila baada ya utesi wa uchaguzi.

**Tatu: mbinu moja wapo ya kuendeleza ukoloni**

Jambo muhimu hapa la kulifahamu ni kuwa kwa kugawanya jamii kwa misingi ya rangi, eneo na kabila, kisha kuja na sura nyengine duni zaidi nayo ni utaifa na uzalendo, yote haya ni miongoni mwa njama anazotumia mkoloni mambo leo kumakinisha athari yake ya kisiasa na kiuchumi katika ulimwengu kwa ujumla na hasa eneo la nchi za Kiislamu. Na hivyo hivyo ndio wakoloni hao walifaulu kuangusha Dola ya Kiislamu ya Uthmaniya. Kupitia mbinu ya kimishenari ndani ya serikali ya Kiislamu ndio wakapenyeza humo sumu za ukabila na utaifa.

Uislamu huondosha ukabila na utaifa na uzalendo:

Jamii ya Kiarabu ilikuwa ikitokota kwenye chungu cha maradhi ya ukabila kwa miaka na mikaka hadi pale ulipokuja Uislamu. Katika kuondosha maovu haya Uislamu ukaanza kutangaza Imani ya kumwamini Mungu Mmoja tu naye ni Allah (swt) muumba wa mbingu na ardhi.

وَمَا أُمِرُوا إِلَّا لِيَعْبُدُوا اللَّهَ مُخْلِصِينَ لَهُ الدِّينَ حُنَفَاءَ
وَيُقِيمُوا الصَّلَاةَ وَيُؤْتُوا الزَّكَاةَ وَذَلِكَ دِينُ الْقَيِّمَةِ

**Nao hawakuamrishwa kitu ila wamuabudu Mwenyezi Mungu kwa kumtakasia Dini, wawe waongofu, na washike sala na watoe Zaka. Na hiyo ndiyo dini madhubuti.** [Al-Bayyina: 5]

Aidha Uislamu ukaeleza bayana kuwa fungamano pekee linapaswa kuwafungamanisha watu wote ni itikadi pevu na wala sio la kikabila. Asema Allah Taala:

يٰأَيُّهَا ٱلَّذِينَ آمَنُواْ لاَ تَتَّخِذُوۤاْ آبَآءَكُمْ وَإِخْوَانَكُمْ أَوْلِيَآءَ
إِنِ ٱسْتَحَبُّواْ ٱلْكُفْرَ عَلَى ٱلإِيمَانِ وَمَن يَتَوَلَّهُمْ مِّنكُمْ
فَأُوْلَـٰئِكَ هُمُ ٱلظَّالِمُونَ

**Enyi Mlioamini msiwafanye baba zenu na ndugu zenu kuwa vipenzi vyenu ikiwa wanapenda ukafiri kuliko Imani.** [At-Tawba: 23]

Hii inamaanisha watu wote waliokubali Uislamu tayari ilitosha wao kuwa kitu kimoja na hakuna tena ukabila, rangi na eneo kutangulizwa mbele ya Uislamu. Mwenyezi Mungu baada ya kuamuru Waislamu kuwa kitu kimoja chini ya itikadi moja akawakataza kugawanyika.

وَاعْتَصِمُوا بِحَبْلِ اللَّهِ جَمِيعًا وَلَا تَفَرَّقُوا وَاذْكُرُوا نِعْمَةَ
اللَّهِ عَلَيْكُمْ إِذْ كُنْتُمْ أَعْدَاءً فَأَلَّفَ بَيْنَ قُلُوبِكُمْ فَأَصْبَحْتُمْ
بِنِعْمَتِهِ إِخْوَانًا وَكُنْتُمْ عَلَى شَفَا حُفْرَةٍ مِنَ النَّارِ فَأَنْقَذَكُمْ
مِنْهَا كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ آيَاتِهِ لَعَلَّكُمْ تَهْتَدُونَ

**Na shikamaneni kwa kamba (Dini) ya Mwenyezi Mungu nyote pamoja, wala msifarakiane. Na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu: vile (zamani) mlivyo kuwa nyinyi kwa nyinyi maadui naye akaziunganisha nyoyo zenu; kwa neema yake mkawa ndugu. Na mlikuwa ukingoni mwa shimo la Moto naye akakuokoeni nalo. Namna hivi Mwenyezi Mungu anakubainishieni aya zake ili mpate kuongoka.** [Aal-Imran: 103]

Isitoshe Uislamu ukashambulia miito ya wale wanaolingania ukabila

Mtume (saw) akasema:
**Sio katika sisi mwenye kulingania ukabila, si katika sisi mwenye kupigania ukabila na wala sio katika sisi mwenye kulingania ukabila**

Kwa kuwa dunia sasa inaelekea kushuhudia mwamko wa kikweli nao ni kurudi kwa maisha ya Kiislamu yakitekelezwa ndani ya serikali yake ya Khilafah,itakuwa mawazo finyu mno kwa harakati zote za Waislamu zinazotamani mabadiliko haya kujifunga na fikra za kizalendo, kitaifa na ukabila.

**Shabani Mwalimu**
**Mwakilishi kwa vyombo vya Habari Hizb ut Tahrir Kenya**

# Matumizi Mabaya ya Teknolojia ya Mawasiliano Ni Athari ya Uhuru Uliopitiliza

Mawasiliano ni jambo la dharura mno katika maisha ya wanadamu. Kupitia kwayo watu huweza kupashana habari muhimu zenye kuleta manufaa katika maisha yao ya kila siku. Katika karne za nyuma mbinu za mawasiliano zilikuwa haba na dhaifu. Miongoni mwazo ni kutuma wajumbe, au upulizaji pembe na uashaji moto kama ishara ya kuonyesha kuwepo kwa habari muhimu. Baada ya kutokea mapinduzi katika teknolojia ya mawasiliano katika nusu ya pili ya karne hii ulimwengu umegeuka kuwa kijiji kidogo ambapo kwa muda wa sekunde moja tu habari huweza kuenezwa kila kona ya ulimwengu.

Mojawapo ya ala za kisasa za mawasiliano ni simu za rununu ambazo hutumika katika mawasiliano ya kila siku baina ya watu pasi na kizuizi cha masafa. Kutokana na kudumu katika uvumbuzi, simu hizi sasa hazitumiki tu katika mawasiliano bali pia katika miamala ya kifedha na kutembea mitandaoni ili kupata huduma mbali mbali.

Miongoni mwa fikra msingi zinazo tukuzwa na mfumo unaotawala leo dunia wa kirasilimali ni mwanadamu kupewa uhuru kamili wa kibinafsi na umilikaji. Mfumo huu hudai kuwa mwanadamu asili yake ni mtu mzuri; uovu wowote unaojitokeza kwake ni kutokana na yeye kunyimwa uhuru kufanya kama apendavyo yeye. Sasa ili asili yake hii iweze kujitokeza, hana budi kudhaminiwa uhuru kamili, na kazi ya serikali ni kulinda na kudhamini kupatikana kikamilifu kwa uhuru wa watu binafsi. Na kwamba saada au furaha ni mtu kufanya bidii kupata starehe za kiwiliwili.

Ni kutokana na uhuru huu ambapo neema hii ya teknolojia ya mawasiliano leo imegeuka kuwa sumu inayo enezwa na kuchafua mabongo ya watu haswa vijana wa Kiislamu, iliyowapelekea kukaa mbali na Uislamu wao kwa kuonyeshwa kuwa kikwazo cha 'furaha' yao. Miongoni mwa maovu yanayofanyika kupitia vifaa hivi vya mawasiliano ni:

**Kwanza: kukithiri kwa uchafu wa zinaa**

Simu leo zimekuwa ni sababu ya vijana kuweza kupata njia rahisi ya kuingia katika mitandao michafu inayo pigia debe munkar huu, ikiwemo ukhanithi na usago, na kuwawezesha kuangalia picha na video za ngono waziwazi na kisha kuwapa mshawasha wa kwenda kuyafanya wanayo yaona humo kivitendo.  Hatima yake imepelekea kutapakaa kwa uovu huu katika jamii au kiasi cha hata wengine kuamua kuichukulia kama njia ya kujikimu kimaisha yenye pato kubwa, kwa kujihusisha na uzinifu.

**Pili: kuenea kwa kamari**

Makampuni ya kamari ya kirasilimali nayo kwa kutumia uhuru huu wa kumiliki yamepatiliza fursa ya maendeleo katika teknologia hii ya mawasiliano kujinufaisha kimapato kupitia kuanzisha michezo hii ndani ya simu za rununu, na tena kwa kiwango kidogo cha pesa ili kurahisisha kushiriki kwake. Kila uchao makampuni kadha wa kadha huibuka kwa lengo la kujitajirisha kupitia kunyonya mamilioni ya watu. Asilimia kubwa ya wanaoshiriki kamari hizi ni vijana kwa kupitia makampuni haya kutumia mchezo wa soka ambao ni kivutio cha vijana wengi.

Haya ni baadhi tu ya maovu ambayo hupatikana kupitia rununu hizi. Licha ya hayo, maovu haya hayapelekei uharamu jumla wa simu hizi kwa kuwa ni chombo kilicho tokamana na sayansi na teknolojia ambayo ni miongoni mwa Madaniyya jumla iliyo vumbuliwa kwa ajili ya manufaa ya wanadamu wote, isipokuwa uharamu unabaki katika namna ya utumizi wake.

Mwanadamu daima hujenga suluki zake na miondoko yake maishani kutokamana na fikra msingi zinazo tawala ubongoni mwake. Fikra hizi aghalabu huzaliwa na kukuuzwa na mfumo unaomtawala mwanadamu huyu. Sasa ikiwa miongoni mwa fikra zinazo kuuzwa na kupigiwa debe na mfumo unaotawala leo wa kirasilimali ni uhuru wa kibinafsi na wa kumiliki uso mipaka, na kwamba serikali daima impe kipao mbele mtu binafsi juu ya jamii, na kwamba bidhaa au huduma yenye thamani kiuchumu ni ile inayo hitajiwa na mtumizi hata kama inaenda kinyume na maadili, twatarajia nini basi isipokuwa muozo na uharibifu? Kwa hayo, mtumizi wa simu au kifaa chochote chengine ili aweze kukitumia kwa njia inayostahiki hana budi basi ubongoni mwake muwe na fikra safi zilizo hifadhika na ufisadi.

Hili kivitendo haliwezi kupatika kwa ukamilifu ikiwa ule mfumo uliozaa na kukuza fikra hizi fisidifu miongoni mwa vijana bado ndio unaotutawala maishani mwetu, kwa kuwa kubakia kwake utaendelea kuhifadhi uovu huu kupitia utoaji leseni kwa mitandao hii na makampuni haya kuendeleza biashara zao, kwa kuona udharura wa kuwepo uhuru wa kibinafsi na wa kumiliki, na hivyo basi kusababisha vijana zaidi kutumbukia katika janga hili.

Ili kukomesha haya, hapana budi basi kung'olewa mfumo huu wa kibepari wa kirasilimali uliopagawa na pato zaidi ya maadili, kwa kujitolea kwa hali na mali kulingania mfumo badali wa Uislamu wenye kukuuza maadili bora kwa raia wake hususan vijana ambao kupitia serikali yake ya Khilafah itakuza maadili mema ya uchaji Mungu miongoni mwa raia wake na kupiga marufuku uwepo wa mitandao au makampuni yanayo kiuka maadili haya ndani ya serikali, hivyo basi kupelekea kudhibiti na kushajiisha utumiaji vyema wa teknolojia ya mawasiliano kwa lengo la kueneza thaqafa ya Kiislamu na kuinua kalima ya Tawheed ya "La Ilaha illallah Muhammadun Rasulullah"

**Masoud Salim Mazrui**
**Mwanachama wa**
**Hizb ut Tahrir Kenya**

# Kashfa ya Ngono ya Westminster Inaangazia Mianya Katika Nidhamu Huru ya Kisekula



**Habari:**

Mnamo Jumatatu tarehe 6 Novemba, viongozi wa vyama vikuu vya kisiasa nchini Uingereza walikutana kujadili mipango ya jinsi ya kukabiliana na mgogoro wa kashfa ya ngono ulioigubika Westminster na kuzitingisha siasa za Uingereza kwa muda wa wiki mbili zilizopita. Walikubaliana kuwepo kwa mpangilio huru mpya wa kushughulikia malalamishi na kuboresha nguvu kazi ili kusaidia waathiriwa wanaosibiwa na dhulma za kimapenzi kutoka kwa wanasiasa na wafanyi kazi wengineo wa bunge. Kwa muda wa wiki mbili, msururu wa tuhuma kuanzia kwa mashambulizi na ubakaji mpaka kwa unyanyasaji wa kimapenzi na kutusiwa na kukejeliwa yameshtakiwa dhidi ya baadhi ya wabunge na wanasiasa wengine wakuu kutoka vyama vyote vya kisiasa, wakiwemo Waziri wa Biashara za Kimataifa, Katibu wa Kwanza wa Serikali, na Waziri wa Ulinzi ambaye alijiuzulu wadhifa wake kutokana na tuhumu hizi. Kashfa hii imeangazia jinsi gani dhuluma za kimapenzi ni tatizo sugu ndani ya kuta za bunge. Kiongozi wa chama cha Labour, Jeremy Corbyn alieleza kuwa "uovu na udhalilifu wa desturi ya dhulma za kimapenzi" umenoga katika Westminster. (Gazeti la Independent)

**Maoni:**

Tabia hii chafu ni moja tu kati ya matunda maovu yanayo tokana na dosari za thaqafa na nidhamu huru ya kisekula iliyokuza mila ya utovu wa heshima kwa wanawake unaofanywa na wanaume wengi pamoja na kusababisha mkorogo katika maangiliano sahihi na halali baina ya jinsia zote mbili. Ule ukweli kuwa unyanyasaji wa kijinsia, mashambulizi na ubakaji yameenea

*Endelea Uk..9*

pakubwa miongoni mwa jamii huru za kiulimwengu, na kuathiri nyanja zote za kimaisha, ikiwemo siasa, vyombo vya habari, taasisi za elimu, sekta ya afya, na jeshi, unapasa kuibua maswali mengi ya dori ya maadili huru na sheria katika kuchangia kusababisha janga hili. Utafiti uliochapishwa mnamo 2016 na Muungano wa Baraza la Wafanyibiashara (Trade Union Congress (TUC)) na mradi wa Everyday Sexism Project uligundua kuwa zaidi ya nusu ya wanawake (52%) nchini Uingereza wamepitia unyanyasaji wa kimapenzi makazini, na miongoni mwa wanawake na wasichana wenye umri kati ya 16-24, kiwango kilicho ripoti unyanyasaji huu wa kimapenzi kiliongezeka mpaka asilimia 63%. Mmoja kati ya wanawake 8 ameripoti kutomaswa kwa dhulma kazini na asilimia 1% wamesema kuwa wamebakwa au kushambuliwa kimapenzi makazini mwao. Yote haya ni licha ya kuwa dhulma ya kimapenzi imeorodheshwa kuwa njia mojawapo ya ubaguzi haramu chini ya Sheria ya Usawa ya 2010 (2010 Equality Act), na kutomaswa kwa dhulma inajumuishwa na sheria kuwa shambulizi la kimapenzi.

Imeangazia ukweli kuwa uimarishaji wa hatua za kinidhamu, mpangilio wa kushughulikia malalamishi na adhabu za kimahakama pekee hayawezi kuwa ndio njia ya kuzalisha 'desturi ya heshima' kwa wanawake. Bali, jamii huru hizi zinahitaji kutambua kwamba kupigia debe uhuru wa kijinsia, pamoja na kuruhusu ngono wazi katika jamii na wanawake kupitia burudani, matangazo ya biashara na sekta nyinginezo pasi na shaka yana athari mbaya ya namna wanaume wanavyo watazama na kuamiliana na wanawake

Zaidi ya hayo, kutoripoti malalamishi ya unyanyasaji wa kimapenzi kwa wanawake wengi kutokana na hofu ya kudharauliwa, kutengwa makazini, au kupoteza kazi zao ni shutma tosha kwa namna hadhi ya wanawake ilivyo shuka miongoni mwa jamii huru. Katika utafiti wa TUC uliotangulia kutajwa, katika kila wanawake wanne kati ya watano walisema kuwa hawaku ripori matukio haya kwa waajiri wao, huku wengi wakihofia kuwa huenda ikaathiri mahusiano yao kazini au hata kutotiliwa maanani. Hofu hii haipaswi kuweko. Katika kashfa hii ya sasa ya Westminster, baadhi ya wanawake wameripoti kuwa walipopeleka malalamishi yao kuhusiana na kudhulumiwa kimapenzi na wabunge au wanachama wakuu wa vyama, malalamishi yao yalitupiliwa mbali chini ya zulia au hata kuvunjwa moyo kutoripoti kadhia hii. Kwa mfano, Bex Bailey, mwanaharakati mwenye ushawishi wa chama cha Labour aliyedai kubakwa katika hafla ya chama mnamo 2011, alisema kuwa alipoelezea uhalifu huu kwa afisa mkuu wa chama hicho aliambiwa kwamba endapo ataripoti tukio hili huenda likamuharibia taaluma yake. Yote haya yanaashiria jinsi gani jamii za kirasilimali, hupatia kipao mbele zaidi kutafuta mamlaka ya kisiasa au faida ya kimapato, kuliko kulinda heshima ya wanawake.

Kuongezea, yaliyoibuka katika majadiliano miongoni mwa jamii huru juu ya kashfa hii ni kuchanganyikiwa juu ya ni nini hasa kinacho jumuisha unyanyasaji wa kimapenzi na ni nini 'ashiki ya kawaida isio hatia' or 'mguso wa kirafiki baina ya wafanyikazi wenza' kama wanavyo uita baadhi. Ubaguzi uliopo ndani ya jamii huru na ukosefu wa mipaka ya wazi katika maingiliano yanayo ruhusiwa na yasiyo ruhusiwa baina ya wanaume na wanawake kutokana na kuifanya akili kuwa chimbuko la usahihi na kosa kwa watu imesababisha kuwepo kwa mkorogo huu. Natija yake, baadhi ya wanawake wanao sibiwa na maneno ya matusi au aina za upapasaji wa kihalifu huchukuliwa kama walio pitiliza kihamaki na hivyo basi kutotiliwa maanani.
Kukinga unyanyasaji wa kimapenzi na mashambulizi dhidi ya wanawake yahitaji imani, maadili na sheria zinazo kuza heshima kwa wanawake na kuhifadhi hadhi yao katika kila daraja ya jamii. Nidhamu ya kijamii ya Kiislamu imekusanya imani, maadili na sheria hizo zinazo wawajibisha wanaume kuwatazama na daima kuamiliana na wanawake kwa heshima. Inaharamisha kuwachukulia wanawake kama vifaa vya ngono au kuwadhalilisha kwa lengo lolote, huku ikiweka wazi kuhifadhi hadhi ya wanawake juu ya maslahi yoyote ya kipesa au ya kimada. Uislamu pia unapinga uhuru wa kijinsia, na badala yake, umeweka mkusanyiko wa sheria zinazo dhibiti imara mahusiano baina ya wanaume na wanawake kuhakikisha kuwa aina zote za maingiliano ya kijinsia, pasi na udhuru wowote, zinafungika katika ndoa pekee. Hii ikiwa ni pamoja na kuweka adhabu kali kwa aina yoyote ya ukiukaji wa hadhi ya mwanamke, ikiwemo hata kutamka neno moja tu linalo vunja heshima yake. Yote haya husaidia kuwepo kwa uhusiano salama na wenye kuzaa matunda baina ya jinsia zote ndani ya jamii, wenye kuwawezesha wanawake kufanya kazi, kusoma, kusafiri na kuishi maisha jumla yasiyokuwa na hofu ya unyanyasaji na mashambulizi.

**Dkt. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake Katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**



# Njia ya Mtume (saw) Kuleta Mageuzi

## Halaqa 7: Kutengwa na Vikwazo kwa Wabebaji Da'wah na Wafuasi Wao

Katika halaqa hii tutazungumzia mbinu ya tatu ambayo Maqureysh walitumia dhidi ya daa'wah ya Mtume (saw) ambayo ni **Kuwatenga na Kuwawekea Vikwazo wabebaji da'wah na wafuasi wao.**

**Suala la Mkataba (Swahifah)**

Maquresh walipoona kuwa Maswahaba wa Mtume (saw) wameshukia mji wa Habasha na wamepata huko amani na utulivu, na Najashiy amewazuia Maqureysh waliokwenda kwake, na Umar ibnul Khatwab amesilimu! Na akawa yeye na Hamzah ibnu Abdul Mutwalib wako pamoja na Mtume (s.a.w) na Maswahaba zake! Na Uislamu unaenea katika makabila, walikusanyika na wakapanga njama kati yao, waandike mkataba ambao watawafunga Bani Hashim na Bani Abdil Mutwalib, Wasiwaolee; wala wasiwaozeshe, Wasiwauzie wala Wasinunue kwao!

Walipoafiqiana juu ya hilo waliandika mkataba, na kuubandika mkataba ndani ya Kaa'bah, sisitizo kwa nafsi zao. Maquresh wakawafungiza Waislamu na Bani Hashim katika shiibi/ (kichaka) cha Abi Talib, na kKutengwa na Vikwazo kwa Waislamu kuliendelea kwa muda wa miaka mitatu (3) mfululizo. Kutengwa na Vikwazo hivyo vikazidi mpaka wakala majani ya miti kwa njaa!

**Kuvunjwa kwa Mkataba:**

Miongoni Mwa Maqureysh kulikuwepo na walioridhia na mkataba huo na wengine waliouchukia, wakaenda mbio kuvunja mkataba wale wanaochukia, na ikawa anayesimamia suala hili ni Hisham Ibnu Amru. Na alikuwa akiwasiliana na Bani Hashim katika kichaka akiwapelekea chakula usiku akiwa amejificha, akaenda kwa Zuhayr bin Abi Umayyah akamwambia: "Ewe Zuhayr!Je waridhia unakula chakula na kunywa maji na kuvaa nguo na kuoa wake, na wajomba zako wako katika hali unayoijua? Hawauziwi wala watu hawanunui, hawaoi, wala hawaozeshwi?" Zuhayr akasema "Ole wako mimi peke yangu nitaweza kufanya nini? Lau kungekuwa na mtu mwengine ningesimama kuuvunja mkataba". Akasema Hisham "Basi umeshapata mtu". Akasema Zuheyr "Ni nani basi?" Akasema Hisham "Mimi". Zuheyr akamwambia "Tutafutie mtu wa tatu".

Akaenda Hisham kwa Mut'im Ibnu Adiy na akasema "Je unaridhia vizazi viwili viangamie katika Bani Abdi Manaf, na wewe ni shahidi juu ya hayo na kuwaunga Maqureysh juu ya dhulma hii?" Akasema Mut'im: "Nitafanya nini mimi peke yangu?" Akasema Hisham "Umeshapata wa pili". Akasema Mut'im "Nani?" Akasema Hisham: "Ni mimi". Akasema Mut'im: "Tutafutia wa tatu". Akasema Hisham "Tayari". Akasema Mut'im "Ni nani?" Akasema Hisham: "Zuhayr bin Abi Umayyah ". Akasema Mut'im: "Tutafutie wa nne".

Akaenda Hisham bin Amru kwa Bakhtariy Ibn Hisham, akamwambia kama alivyomwambia Mut'im Ibn Adiy Akasema: "Je kuna yeyote atakaye saidia hili? Akasema Hisham: "Ndio". Akasema Amru: "Ni nani?" Akasema Hisham: "Ni Zuhayr Ibn Umayyah na Mut'im Ibn Adiy na mimi niko pamoja nao". Akasema Mut'im: "Tutafutie wa

*Endelea Uk..11*

tano".

Akaenda kwa Zam'ah Ibn AL-Aswad akamzungumzisha, akamweleza ukuruba wao na haqi yao, Akasema Zam'ah: "Je hili jambo unalonilingania kuna mtu yeyote?" Akasema Hisham: "Ndio". Akamwelezea wale jamaa, wakaahidiana usiku kukutana "HUJUN" ni Jabali liko juu katika mji wa Makkah wakakutana huko na wakakubaliana juu ya kuuvunja mkataba, Akasema Zuheyr: "Mimi nitawaanzia na nitakuwa wa kwanza atakaye zungumza".

Walipopambaukiwa wakaenda katika maskani zao na akaja Zuheyr Ibnu Umayah akiwa amevalia vizuri, akatufu Kaa'bah mara saba, kisha akawaelekea watu. Akasema: "Enyi watu wa Makkah! Je, sisi tunakula chakula, na kuvaa nguo, na Banu Hashim wanaangamia hawauziwi wala watu hawanunui kwao! Wallahi sitokaa mpaka huu mkataba wa dhulma uraruliwe". Akasema Abu Jahl aliyekuwa katika kipembe cha msikiti: "Umesema uongo Wallahi hauraruliwi!"

Akasema Zam'ah Ibn Al-Aswad: "Wallahi wewe ndiye muongo zaidi hatukuupitia mkataba huu ulipoandikwa!" Akasema Abu Bakhtariy Ibn Adiy "Mumesema kweli nyie wawili na ni muongo atakayesema kinyume na hivyo! Tunajitenga kwa Allah kutokana na mkataba huu na kilicho andikwa ndani yake!"

Akasema Hisham Ibn Amru kama hivyo! Akasema Abu Jahl "Hili jambo limepangwa usiku watu wameshauriana mahala pasipo hapa". Akasimama Mut'im ili akaurarue mkataba akakuta mchwa wameula isipokua "BISMIKALLAHUMMA" kwa jina lako ewe Mola hapo tu ndio hapakuliwa

Na kwa Njia hii mkataba ukavunjwa, Akatoka katika kichaka Mtume (saw) na aliokuwa pamoja nao. Hakika Maqureysh waliona muujiza mkubwa miongoni mwa miujiza ya Utume wake lakini wao waliipa nyongo na wakazidisha ukafiri juu ya ukafiri wao:

Kama alivyoelezea Allah Ta'ala:

وَإِنْ يَرَوْا آيَةً يُعْرِضُوا وَيَقُولُوا سِحْرٌ مُسْتَمِرٌّ

**Na wakiona Ishara hugeuka upande na husema: Huu uchawi tu unazidi kuendelea.** [Al-Qamari: 2]

Itaendelea katika UQAB Toleo 12…In Shaa Allah.




# SWALI / JAWABU: Matokeo ya Kisiasa Katika Mkoa wa Catalonia!

**Swali**

Shirika la habari la BBC liliripoti afisi ya Waziri Mkuu wa Uhispania Mariano Rajoy, leo (19/10/2017), ikisema: "Baraza la Mawaziri huenda likakutana kukifanyiakazi kifungu cha 155 cha katiba, kuliruhusu kuchukua mamlaka ya kuendesha eneo hili… Kiongozi wa serikali ya eneo la Catalonia, Carles Puigdemont, alikuwa ametuma barua kwa serikali ya Uhispania, akitishia kuwa bunge la eneo hilo litapitisha kura ya maamuzi juu ya uhuru wa kujitenga na Uhispania ikiwa Madrid itaweka kizuizi kwa mazungumzo na kuendelea na unyanyapaa wake." Baada ya kura ya maamuzi ya mnamo 1/10/2017, Raisi wa eneo hilo alitangaza mnamo 10/10/2017 mbele ya bunge la eneo hilo kujitenga kutoka kwa Uhispania, lakini akafanya utekelezaji wa hili kuwa wazi kwa mazungumzo. Sasa, ni kwa nini eneo hili lilifanya kura hii ya maamuzi licha ya upinzani kutoka kwa dola ya Uhispania; mfalme wake, serikali yake na mahakama yake ya katiba?

Msimamo wa kimataifa ni upi juu ya hili? Na ni upi uwezekano wa kutekelezwa kwa uhuru wa Catalonia? Jazakum Allah Khairan.

**Jibu**

Ili taswira hii iwe wazi na kupata jibu sahihi zaidi la swali hili, tutaitathmini upya hali halisi ya Catalonia, harakati zake kabla ya kujitenga, na kisha yanayojiri baada ya kura ya maamuzi, tutataja msimamo wa kimataifa juu ya hili, na baadaye, tutadadisi uwezekano wa kutekelezwa kura hii ya maamuzi:

**Kwanza: Historia na hali ya kijiografia ya Catalonia:**

Eneo hili linapatikana Kaskazini Mashariki mwa Uhispania lenye ukubwa wa kilomita 32.1 mraba, ambayo ni asilimia 8 ya Uhispania, Barcelona ikiwa ndio mji mkuu wake. Eneo hili linajumuisha mikoa minne, kwa majina: Barcelona, Girona, Lleida na Tarragona, jumla ya idadi ya wakaazi ni milioni 7.5, inayo wasilisha asilimia 16 ya wenyeji wa Uhispania ambalo ni miongoni mwa maeneo kumi na saba yenye uhuru wa kujitawala wenyewe nchini humo.

Uislamu umeangaza Catalonia tangu mwaka wa 95 Hijria wakati wa kufunguliwa kwa Andalusia. Utawala wa Kiislamu ulipo malizika, eneo hili liliendelea kuwa eneo huru, baadaye Uhispania ukaliunganisha nayo kwa nguvu mnamo 1714 Miladi. Watu wa mkoa huu hawakukubali hili na walidumu kung'ang'ana kujikomboa kutokana na uvamizi huu wa Uhispania. Mnamo miaka ya 1930, vita vya wenyewe kwa wenyewe vilizuka baina ya serikali kuu ikishirikiana na serikali mshirika wake inayo jitawala wenyewe ya Catalonia upande mmoja, na jeshi la Franco upande wa pili. Baada ya ushindi wa jeshi la Franco, Franco aliwahangaisha wana Catalan, kuzuia lugha yao kuwa lugha rasmi ya eneo hilo, kupiga marufuku kusomeshwa lugha ya Catalan mashuleni, na kuwanyima wa-Catalan kitambulisho. Baada ya kuanguka kwa utawala dhalimu wa Franco, kura maarufu ya maamuzi ilifanywa huku asilimia 30 ya kura hizo zikipendelea katiba ya Uhispania inayo pendekeza umoja wa nchi na haki ya kujitawala wenyewe kwa makabila, jamii za walio wachache na mikoa ya Uhispania. Mnamo 1979, wenyeji wa Catalonia kwa mara nyengine tena walijipatia haki ya kujitawala wenyewe, na hii ndio iliyopelekea kutambuliwa kwa lugha ya Kihispania na Catalan kama lugha rasmi za eneo hili.

Baada ya hapo, harakati za kujitenga za Catalan zilipoa moto mpaka mwanzoni mwa karne hii ambapo zilianza kuibuka tena kidogo kidogo.

**Pili: Hatua za Harakati za Sasa za Catalan:**

1. Harakati hizi zilianza mnamo 2006 kwa kupitishwa sheria mpya ya kujitawala wenyewe na ilipigiwa kura na watu kwa lengo la kupanua mamlaka ya kujitawala wenyewe ya eneo hilo. Sheria hii ililifafanua upya taifa la Catalonia. Mnamo 2010, Mahakama ya Katiba ya Uhispania iliifuta sheria hii jambo lililo pelekea maandamano chini ya mwito "Sisi ni taifa, tunajiamulia". Mnamo Novemba 2012, kura ya maamuzi ya shangwe ilifanywa iliyopigia kura ya kujitenga na dola ya Uhispania. Mnamo Januari 2015, Waziri Mkuu wa Catalonia, Artur Mas, alitangaza kufanyika kwa uchaguzi wa ghafla wa aina ya kura ya maoni mnamo Septemba ya mwaka huo huo. Uchaguzi huu wa mapema ulifanywa na harakati ya kitaifa inayolingania kujitenga ikashinda viti vingi 72 kwa viti 63 ilivyoshinda vyama vinavyo pinga kujitenga. Walio wengi bungeni mnamo Novemba 2015 waliweza

*Endelea Uk..13*

kuchapisha mswada unaotangaza mwanzo wa "Mchakato wa Catalonia kufikia hatua ya serikali huru". Serikali ya Uhispania ilikata rufaa kwa mswada huo katika Mahakama ya Katiba ambayo iliikubali rufaa hiyo.

2. Mnamo 9/6/2017, wakati ambapo hatua hizi zilipamba moto na kuchukua muelekeo imara, Raisi wa serikali ya Catalonia, Carles, alitangaza kwamba "kura ya maoni ya kujitenga kwa eneo hili kutoka kwa Uhispania itafanyika mnamo 1/10/2017 na kwamba serikali itauliza katika kura hii ya maoni swali lifuatalo: "Je, unataka Catalonia iwe dola huru kwa muundo wa jamhuri?" (Novosti, 9/6/2017). Siku iliyofuatia, serikali ya Uhispania ikatangaza kwamba itazuia jaribio lolote la kujitenga kwa Catalonia. Mnamo 6/9/2017, bunge la Catalonia likapitisha sheria inayoweka msingi wa kura ya maamuzi ya kujitenga kwa eneo hilo kutoka kwa dola ya Uhispania. Waziri Mkuu wa Uhispania, Mariano Rajoy, akasema: "Serikali ya Uhispania huenda ikatumia nguvu za kikatiba kusitisha mamlaka ya kujitawala wenyewe ya Catalonia na hivyo basi kulizuia eneo hili kutokana na kujitenga kutoka kwa Uhispania". Mahakama ya Katiba ya Uhispania ikajibu mnamo 8/9/2017 kusitisha kura hii ya maamuzi mpaka itakapo toa hukumu ya uhalali wake kikatiba.

3. Licha ya hayo, kura hii ya maoni ikafanywa mnamo Oktoba 1, 2017 kama ilivyo pangwa. Matokeo yakawa kwamba asilimia 90 ya wapiga kura, ambayo ni asilimia 43 ya wakaazi wote, wakataka kujitenga kutoka kwa Uhispania na kuwa huru. Mfalme wa Uhispania, Philippe VI, akatoa hotuba mnamo Oktoba 3, 2017 baada ya kura hiyo ya maamuzi, huku akiita "isiyo halali na isiyo ya kidemokrasia", lakini gavana wa eneo hilo akasema: " Atatangaza rasmi uhuru huu mwishoni mwa wiki hii au mwanzoni mwa wiki ijayo". Akasema: "Mfalme amekataa jukumu la kuwa mpatanishi alilopewa na katiba ya Uhispania" (BBC 3/10/2017). Inaonyesha kuwa Uhispania imefedheheka. Haikuweza kuzuia mchakato wa kura ya maamuzi, kwa hivyo imechukua hatua za kuiwekea vikwazo iliyopelekea kujeruhiwa kwa watu 893 kutokana na ghasia kati ya majeshi ya usalama na wapiga kura. Hili limepelekea kuibuka kwa rai jumla dhidi yake, na ikawa basi inatafuta njia nyengine za kuzuia kutangazwa kwa uhuru. Kwa hivyo, ikaanza kutumia vita vya kiuchumi dhidi ya eneo hili; taasisi kuu za kifedha na makampuni yakatangaza kuondoka kwao Catalonia, na benki ya tatu kwa ukubwa nchini Uhispania, CaixaBank, mnamo 6/9/2017 ikatangaza uamuzi wake wa kuyaondoa makao yake makuu na kuyapeleka nje ya jiji la Barcelona, mji mkuu wa Catalonia. Mnamo 8/10/2017, maelfu ya wanaopinga kujitenga waliandamana barabarani nchini Uhispania kujenga msukumo wa upinzani ndani ya Catalonia.

4. Raisi wa eneo la Catalonia, Carles, alitangaza mbele ya bunge mnamo 10 Oktoba 2017, uhuru wa mkoa wa Catalonia lakini akaakhirisha utabikishaji wake. Alisema: "Nachukua mamlaka ya watu kutangaza Catalonia kuwa dola huru katika muundo wa jamhuri, naliomba bunge kusitisha utabikishaji wa tangazo hili la uhuru kwa wiki chache kufungua mwanya wa mazungumzo".

Lakini, hakufikia kiwango cha kuliunga mkono bunge kutangaza tangazo hilo la uhuru. (Euro News, Reuters 10/10/2017). Hii yamaanisha kwamba hakutaka kujifedhehesha kwa kutangaza kujitenga kwa sababu anajua kuwa kufikia hili sio rahisi. Kwa hivyo, aliuacha mlango wazi kwa ajili ya majadiliano na dola ya Uhispania kuepuka migongano. Eneo hili, bado limo ndani ya Uhispania, bali tatizo la eneo hili linasalia kuwa hai na lenye kulewa lewa shingoni mwa Uhispania na Muungano wa Ulaya mpaka dhurufu zitakapo ruhusu na uhuru kupatikana.

**Tatu: Msimamo wa kimataifa juu ya matukio ya Catalonia.**

Hapa, tutataja misimamo ya nchi zenye msemo, yaani, Muungano wa Ulaya na Amerika, pamoja na msimamo wa Umoja wa Mataifa ambao unaathiriwa pakubwa na msimamo wa Amerika:

1. Msimamo wa Ulaya ulikuwa wazi dhidi ya kura hii ya maamuzi na uhuru wa Catalonia. Ujerumani, Ufaransa na Muungano wa Ulaya ziliunga mkono msimamo wa serikali ya Uhispania. Naibu wa Waziri wa Kigeni wa Ujerumani alisema kuwa: "mambo yanayo endelea eneo la Catalonia ni ya kutia wasiwasi na kujitenga sio suluhu. Kujitenga hakutatui matatizo yoyote. Wanachama wote wa Muungano wa Ulaya wanapaswa kuheshimu na kujifunga barabara na muongozo na kanuni za utiifu kwa sheria na demokrasia… mizozo ya kisiasa ndani ya Muungano wa Ulaya inapaswa kutatuliwa kupitia mazungumzo badala ya ghasia barabarani." (Reuters, 2/10/2017). Ufaransa imetangaza msimamo wake kupitia Waziri wake wa masuala ya Ulaya, Nathalie Loiseau, kwamba "Ufaransa haitaitambua Catalonia ikiwa eneo hili la Uhispania litatangaza uhuru kipeke yake… Ili uhuru utambuliwe – na ambao sio jambo linalojadiliwa – natija itatayo jitokeza kwa haraka itakuwa ni (Catalonia) moja kwa moja itajiondoa katika Muungano wa Ulaya" (Reuters, 9/10/2017). Raisi wa Tume ya Ulaya, Jean-Claude Juncker, alitangaza msimamo wa muungano huo kuwa "unaotaka kuheshimu maamuzi ya serikali ya Uhispania na Mahakama yake ya Katiba". Huku Raisi wa Baraza la Ulaya, Donald Tusk, akiandika katika mtandao wa Twitter mnamo 2/10/2017, akisema: "Kwa kushirikiana naye (Waziri Mkuu wa Uhispania, Mariano Rajoy) kimaoni ya kikatiba, nimesihi kutafutwa kwa njia za kuepuka mzozo zaidi na utumiaji nguvu".

2. Ama kuhusu msimamo wa Amerika, unaonyesha kuwa serikali ya Catalonia na Raisi wake wameshajiishwa na kuungwa mkono na Amerika. Msemaji wa idara ya

Endelea Uk..14

Amerika, Heather Nauert, alisema: “Amerika inachukulia kura hii ya maamuzi kama jambo la ndani la serikali ya Uhispania na hatunge taka kuingilia. Tutaiwacha serikali yenyewe na watu wake kutatua, na tutafanya kazi na serikali yoyote au utawala wowote utakao zaliwa kutokana nayo” (Gazeti la Misri la Al-Fajr, 16/9/2017). Sentensi hii ya mwisho inachukuliwa kuwa uidhinishaji wa Amerika wa kura hii ya maamuzi na uhuru. Kwa sababu inasema: “tutafanya kazi na serikali yoyote au utawala wowote utakao zaliwa nayo”; yaani, tutalitambua eneo la Catalonia endapo litapata uhuru. Gazeti la Uhispania la “El País” limesema kwamba “raisi wa eneo la Catalan, Carles Puigdemont, alizichukulia taarifa za msemaji wa Amerika kumaanisha kuwa Amerika ina heshimu matakwa ya watu wa Catalonia na matokeo ya kura ya maamuzi.” Kwani inajulikana kuwa Amerika inalenga kuvunja Muungano wa Ulaya kwa kutangaza kuunga mkono kwake Uingereza kujiondoa kutoka kwa muungano huo na kushajiisha hilo kwa nchi nyenginezo za Ulaya, au kwa uchache inataka kuukalia katika mambo yake ya ndani na katika harakati za kujitenga ili muungano huu na nchi zake kuu zisiweze kushindana na Amerika au kuiharibia katika kadhia za kimataifa. Kwa hivyo, kushajiisha harakati hizo za kujitenga ni kwa ajili ya maslahi yake. Na msimamo huu una kinzana na msimamo wake kuhusu kura ya maamuzi ya Kurdistan na uhuru wake ambayo inaipinga kwa nguvu na kuikataa na imezisukuma nchi zilizoko eneo hilo kuanzia Iraq mpaka Iran na Uturuki kupinga na kuikataa vile vile na kumshinikiza Barzani kwa sababu hili halina maslahi naye kwa sasa, hususan kwa kuwa (Amerika) ndiyo yenye athari kubwa nchini Iraq. Uingereza ndiyo iliyompa maagizo kibaraka wake Barzani kuchukua hatua hii ya kuivuruga Amerika ili kuleta takhfifu ya kuondolewa kwa vikwazo vya Amerika vinavyo tekelezwa na Saudi Arabia na Misri juu ya Qatar ambayo ni kibaraka wa Uingereza.

3. Ama kuhusu msimamo wa Umoja wa Mataifa, unao tawaliwa na Amerika, msimamo wake kuhusiana na kadhia ya Catalonia ni kushajiisha kupatikana uhuru wake. Katibu Mkuu wake, Antonios Guterich, alizungumza “matarajio kwamba taasisi za kidemokrasia za Uhispania zitapata suluhu ya mgogoro kati ya wanaharakati wa Catalonia wanaotaka kujitenga na serikali ya kitaifa.” Msemaji wa raisi katika kikao cha 72 cha Kongamano Kuu la Umoja wa Mataifa alisisitiza kuwa “haki ya watu kutaka kujiamulia wenyewe ni haki msingi, huku akitaja haja ya kutekelezwa haki hii pasi na kukiuka msingi wa heshima wa eneo la nchi hii na kupitia itifaki baina ya pande husika” (Associated Press, 3/10/2017). Hili laashiria kwamba Umoja wa Mataifa unapigia debe uhuru wa Catalonia huku ukipinga kura ya maamuzi ya eneo la Kurdistan na uhuru wake kutokana na athari iliyo nayo Amerika katika maazimio ya Umoja wa Mataifa.

Ni wazi kutokana na misimamo hii kuwa harakati za hivi karibuni za Catalonia katika kadhia ya kura ya maamuzi zimeshajiishwa na Amerika kwa sababu Amerika ana hamu ya kuyaharibu mazingira ya Ulaya, hususan katika enzi za Trump, na linalo ufanya mtazamo huu kuwa wenye nguvu zaidi ni misimamo na taarifa zilio tangulia kutajwa hapo juu.

**Nne: uwezekano wa kutekelezwa kujitenga huku:**

Hili si rahisi kutokea angaa kwa mustakbali wa hivi karibuni, na hakuna shaka kuwa Amerika inatambua hili, na ushajiishaji wake kwa harakati za Catalonia ni kwa lengo la kuharibu mazingira barani Ulaya na kulishughulisha nayo kama hatua za mwanzo za mpango wa muda mrefu wa kuuvunja Muungano wa Ulaya. Zaidi ya hayo, kuna sababu nyenginezo zinazo ifanya Uhispania kushindwa kukubali kujitenga kwa Catalonia kwa njia yoyote ile sababu mbili kuu zikiwa:

1. Eneo hili, licha ya udogo wake, huzalisha asilimia 20% ya utajiri wa kitaifa (GNP) wa Uhispania, linadhibiti asilimia 70% ya uchukuzi na mawasiliano yanayo husiana na biashara ya kigeni ya Uhispania na kuzalisha thuluthi moja ya viwanda vya Uhispania, na ndiyo sababu wakaazi wa Catalonia huitakidi kuwa wanazalisha zaidi kuliko wanacho pokea. Na serikali ya Uhispania inawatoza ushuru mkubwa unaofikia kiwango cha asilimia 10% ya uzalishaji wa eneo zima; yote haya yanatilia mkazo vilio na ari ya kujitenga. Kwa upande mwengine, Uhispania inakumbwa na matatizo ya kiuchumi, bajeti dhaifu ya umma, upungufu mkubwa wa matumizi ya bajeti na ongezeko la kiwango cha ukosefu wa ajira, ikiongezewa na uchache wa suluhu. Uchumi wa Catalonia ni jambo muhimu katika kusuluhisha matatizo ya kiuchumi.

2. Zaidi ya hayo, kujitenga kwa Catalonia kutapelekea kugawanyika zaidi kwa Uhispania na sehemu nyenginezo kwa sababu uhuru wa Catalonia utakuwa ni kichocheo cha nchi ya Basque ya Uhispania ambayo imewahi kutafuta uhuru awali. Nchi ya Basque imeunga mkono hatua ya Catalonia, ishara kuwa nchi ya Basque huenda ikalingania kujitenga kwa mara nyengine tena kwa kuwa ari ya wanaharakati ya kujitenga haija fifia bado. “Nchi ya Basque tayari imetangaza hamu ya kujitenga kutoka kwa eneo la Uhispania kuanzia mwaka ujao” (Siyasa Post 24/9/2017). Ni eneo lililo kumbwa na ghasia na vifo vya mamia ya watu ambapo harakati ya ETA imekuwa ikiongoza mchakato wa kisilaha wa kujitenga kwa miaka mingi mpaka makubaliano ya kusitisha mapigano yalipo fanyika miaka mitatu iliyopita na harakati hii kutupilia mbali silaha zake baada ya kupata mamlaka ya eneo hili. Kwa hivyo, kujitenga kokote kutakako tokea katika mkoa mojawapo kwa kiasi kikubwa kutafuatwa na mikoa mengine. Waziri wa Haki wa Uhispania ameonya juu ya hili na alinukuliwa akisema: “Nina wasiwasi mkubwa kuwa uhuru wa Catalonia utafikisha hatima dola ya Uhispania, kwa sababu uhuru wa Catalonia huenda ukaleta “athari

***Endelea Uk..15***

ya kichocheo" katika eneo zima" (Al Jazeera, 2/10/2017).

Uhispania, hivyo basi, haiwezi kukubali kwa njia yoyote kugawanywa kwa eneo la Catalonia, bali, inatishia kukifanyiakazi kifungu cha 155 kuzuia haki ya kujitawala wenyewe kwa eneo hili ikiwa itashindwa kuzuia kujitenga kwa njia yoyote kama ilivyo fahamika kutoka kwa afisi ya Waziri Mkuu wa Uhispania, na kama ilivyo ripotiwa na shirika la habari la BBC mnamo 19 Oktoba 2017.

3. Zaidi ya hayo, Muungano wa Ulaya unakaribia kuporomoka endapo fikra ya kujitenga itaenea maeneo yake, hususan ikiwa kujitenga huku (kwa Catalonia) kutapatikana. Hii ni kwa sababu zipo harakati za kujitenga nchini Ufaransa, ambapo eneo la Catalonia na nchi ya Basque zimegawanyika baina ya Ufaransa na Uhispania, na kunayo harakati ya kujitenga katika kisiwa cha Corsica kinacho taka kuwa huru na Ufaransa na kinasubiri tu mafanikio ya eneo la Catalonia kuchukua hatua.

Pia, kunazo harakati za kujitenga nchini Italia, Belgium na kwengineko, ambazo zinatishia mshikamano wa Muungano wa Ulaya unao kumbwa na migogoro mingi na tishio kutoka kwa harakati za kitaifa za kutaka kujiondoa kutoka kwa muungano huo kama ilivyo tokea kwa Uingereza almaarufu kama Brexit.

Yote haya yanafanya uwezekano wa kutabikishwa kujitenga huku kutokuwa na uhakika na kuwa vigumu sana, kwani ni tishio, sio tu kwa Uhispania pekee, bali kwa Muungano mzima wa Ulaya.

Inaonyesha kuwa raisi wa eneo hili ameanza kutambua hili kama alivyo jiona karibu ya kutengwa na mpaka eneo lenyewe, kwani alipingwa na halaiki ya watu. Kwa hivyo, uamuzi wa kutangaza uhuru hauku kamilika kwa kuwa raisi wa eneo hili aliakhirisha utabikishaji wake mpaka majadiliano ya kupata uhuru mkubwa zaidi wa eneo pamoja na kubuni fursa na kusubiri dhurufu muwafaka za kupata uhuru siku za usoni, ima hili liwe kwa ajili ya hadhi ya Uhispania au hadhi ya Muungano wa Ulaya. Hata Amerika iliyo ushajiisha imepunguza kasi ya kuunga mkono ilipo ona msimamo mkali wa Uhispania iliyo ungwa mkono na Muungano wa Ulaya. Hiyo ndio sababu ya Raisi Trump kusema wakati wa mkutano wake na Waziri Mkuu wa Uhispania, Rajoy, aliye kwenda Amerika kuvinjari rai yake juu ya uhuru wa Catalonia, "Tunaamiliana na nchi kubwa kweli kweli, na haina budi ibakie kuungana" (Gazeti la Misri la Ashorooq 27/9/2017).

Na Raisi wa eneo hili atatambua kuwa Trump ni kama shetani katika ahadi zake

**(يَعِدُهُمْ وَيُمَنِّيهِمْ وَمَا يَعِدُهُمُ الشَّيْطَانُ إِلَّا غُرُورًا)**
**Anawaahidi na anawatia tamaa. Na Shet'ani hawaahidi ila udanganyifu.** [An-Nisaa: 120]

Hata hivyo, Amerika itaendelea kuuhujumu Muungano wa Ulaya, na itawatafuta wale watakaoitikia ahadi zake barani Ulaya!

Tano: Hivyo basi, utaifa humomonyoa wamiliki wa mfumo wa kirasilimali, hususan Ulaya, kuuzorotesha na kudhaifisha umoja wake, mshikamano na kazi yake ya kisiasa ng'ambo. Kwa sababu, mfumo wa kirasilimali haukuweza kushughulikia suala la utaifa, na wala hautaweza, ni mfumo ulio feli mbali na kuwa ni batili kutokana na msingi wake wa kutenganisha dini na maisha. Na ni fisidifu kwa sababu demokrasia yake inayo dhibitiwa na wamiliki wa rasilimali ambao hujinyakulia vyeo na fursa kupitia jina lake na kupitia matumizi mabaya ya sheria. Pia ni mfumo dhalimu kwa sababu hupiga vita dini na wale wanao shikamana nayo, na kuwepo ubaguzi baina ya watu kwa misingi ya dini au ukabila. Hili limejitokeza nchini Amerika na Ulaya na wala huu si ufahamu wa kimakosa wala kutia chumvi katika uoni.

Sheria zote zilizotungwa na mwanadamu haziku takata kutokana na dhulma hii, ugandamizaji na ufisadi wala kutokana na utumwa wa nchi na watu wake. Ni Uislamu pekee, ambao umeteremshwa na Allah, Mola wa walimwengu, unao simamisha haki na uadilifu miongoni mwa watu na kuweka sawa mambo yao,

(أَلَا يَعْلَمُ مَنْ خَلَقَ وَهُوَ اللَّطِيفُ الْخَبِيرُ)
**Asijue aliye umba, naye ndiye Mjua siri, Mwenye khabari?** [Al-Mulk: 14]

Uislamu ndio ulio wayeyusha watu kuwa umma mmoja na kuondoa migawanyiko ya kitaifa na ya kikabila na uadui kama ulivyo haramisha hamasa za kitaifa na miundo yote ya Asabiyya na kuipiga vita vya kudumu.
Uislamu ndio unao simamisha uadilifu miongoni mwa watu katika uchungaji wa mambo yao bila ya ubaguzi wa kidini, kikabila, rangi, jinsia au jengine lolote, bali watu wote huchukuliwa kuwa sawa; huamiliwa kwa uadilifu mbele ya mahakama chini ya kivuli cha dola ya Khilafah Rashidah.

Imam Ahmad ameripoti katika Musnad yake: Ismail amepokea kutoka kwa Said al-Jurairi kutoka kwa Abi Nadra kutoka kwa wale waliomsikiza Mtume wa Allah (saw) katikati ya siku za at-Tashriq kwamba Mtume wa Allah (saw) amesema:
**يَا أَيُّهَا النَّاسُ، أَلَا إِنَّ رَبَّكُمْ وَاحِدٌ، وَإِنَّ أَبَاكُمْ وَاحِدٌ، أَلَا لَا فَضْلَ لِعَرَبِيٍّ عَلَى عَجَمِيٍّ، وَلَا لِعَجَمِيٍّ عَلَى عَرَبِيٍّ، وَلَا أَحْمَرَ عَلَى أَسْوَدَ، وَلَا أَسْوَدَ عَلَى أَحْمَرَ، إِلَّا بِالتَّقْوَى أَبَلَّغْتُ، قَالُوا: بَلَّغَ رَسُولُ اللَّهِ...**
"Enyi watu, Mola wenu ni mmoja, baba yenu ni mmoja. Hakuna fadhla kwa muarabu juu ya asiye kuwa muarabu wala asiye kuwa muarabu juu ya muarabu, wala kwa mwekundu juu ya mweusi wala kwa mweusi juu ya mwekundu isipokuwa kwa uchaji Mungu (Taqwa). Je nimefikisha ujumbe?" Wakasema, "Mtume wa Allah amefikisha ujumbe."

Hii ndio haki:

**(فَماذا بَعْدَ الْحَقِّ إِلاَّ الضَّلالُ فَأَنَّى تُصْرَفُونَ)**
**"Na kipo kitu gani baada ya haki, isipokuwa upotovu tu? Basi huwaje mkageuzwa?"** [Yunus: 32]

# Mgogoro wa Zimbabwe ni Njama ya Uingereza ya Kubadilisha Vibaraka Wake na Kudumisha Hali Halisi

**Habari:**

Zimbabwe inakabiliwa na mgogoro wa kisiasa wa chama tawala cha Zanu-PF, kama maonyesho ya umma juu ya ni nani anaye tarajiwa zaidi kumrithi Raisi Robert Mugabe. Kikwazo kilichopo kwa sasa ni baina ya kundi la vijana, wenye utiifu kwa mkewe, Grace Mugabe, na waliokuwa wapiganaji wa ukombozi, wenye utiifu kwa Emmerson Mnangagwa, makamu wa raisi aliyefutwa kazi wiki iliyopita. [Aljazeera]

**Maoni:**

Eneo la Kusini mwa Rhodesia lililo badilishwa jina kuwa Zimbabwe mnamo 18 Aprili 1980 baada ya kupewa uhuru bandia na bwana wake mkoloni Uingereza. Lakini ukweli ni kuwa Uingereza kama dola yenye nguvu zaidi duniani ambayo ilishuhudia hasara kubwa baada ya Vita vya Pili vya Dunia iliyo ifanya kurekebisha sera yake ya kigeni kupitia wadadisi wake wa kina. Matokeo yake yakawa ni kuchora mapendekezo ya kuhakikisha kuwa Uingereza ina makinika moja kwa moja katika kudumisha msimamo wake wa kiulimwengu nyumbani huku ikisimamia koloni zake kwa njia isiyo ya moja kwa moja kwa kupitia vibaraka wake alio wachagua. Hii itatoa fursa kwa Uingereza kuficha njama zao nyuma ya pazia huku uhakika ukiwa wao ndio wenye amri juu ya vibaraka hao watiifu wanao tawala kwa baraka na muongozo wao. Hii ikimaanisha kuwa sera za koloni zao za kindani na kinje zitaundwa kutokana na matakwa ya bwana Uingereza.

Ama kuhusu Zimbabwe, Waingereza walimchagua Robert Gabriel Mugabe anayetoka katika kabila kubwa zaidi la Shona nchini Zimbabwe ambaye walimpa mafunzo na kumuajiri katika taasisi zao ndani ya nchi pamoja na ng'ambo kama mwalimu. Kisha baadaye kumnyanyua daraja kuwa kama mwanamapinduzi na mwanasiasa kwa kumuhukumu kifungo cha miaka 10 gerezani kuanzia 1964 mpaka 1974. Wakati wa kuachiliwa kwake alikimbilia Msumbiji na kuasisi uongozi wake na kusimamia chama cha ZANU ambacho alikuwa mwenyekiti wake kwa miaka mitano kuanzia 1975 – 1980.

Kisha baadaye baada ya kufanywa 'uchaguzi mkuu' wa kisanii na Mugabe kushinda Februari 1980; Waingereza walimtawaza Mugabe kuwa Waziri Mkuu wa kwanza wa Zimbabwe mnamo 18 Aprili 1980 ambapo alitawala kwa muda wa miaka saba. Mugabe alianza kumhudumia bwana wake kwa ikhlasi na kwa bidii; kwa mfano kati ya mwaka wa 1982 na 1985 aliuvunja vunja upinzani ulioongozwa na chama cha Zimbambwe African Peoples Union (ZAPU). Hii ni baada ya wito wa Mugabe wa kulingania maridhiano kati ya makabila kushindwa kusitisha kuzorota kwa mahusiano kati ya makabila na kukua kwa chuki dhidi ya wazungu. Zaidi ya watu 10,000 waliuwawa na jeshi la Mugabe wengi wao wakiwa ni raia wa kabila la Ndebele walio kuwa wakiongozwa na Joshua Mqabuko Nyongolo Nkomo kama kiongozi na mwanzilishi wa chama cha ZAPU ambaye pia anatoka katika kabila la Ndebele (Kalanga).

Bwana mkoloni akapanga njama za kumtuza Mugabe kwa kazi yake nzuri. Mnamo 22 Disemba 1987, wakaviunganisha vyama vya ZANU na ZAPU na kuunda chama cha Zimbabwe African National Union – Patriotic Front. Waanzilishi wa chama cha ZANU-PF walikuwa ni Mugabe na Joshua; na wenyekiti walikuwa Emmerson Mnangagwa na Phelekezela Mphoko. Mnamo 31 Disemba 1987, Robert Mugabe akatawazwa kuwa raisi wa kwanza wa Zimbabwe na ili kuhakikisha kuwa mpinzani wake Joshua Nkomo anawekwa chini ya uangalizi, akafanywa kama makamu wa raisi asiye na mamlaka yoyote.

Mugabe amekuwa mamlakani kwa muda wa miaka 37 mtawalia akimhudumia Mmagharibi 'bwana mkoloni' kwa ustadi; kile ambacho kimekuwa kikiumisha kichwa Uingereza ni nani miongoni mwa vibaraka wake wengi atakaye mrithi kibaraka wao. Ikizingatiwa kuwa watu wanataka mabadiliko kutokana na maendeleo duni ya kijamii na ya kiuchumi. Mwito wa mabadiliko una ongozwa na Morgan Tsvangirai kinara wa chama cha Movement for Democratic Change – Tsvangirai. Morgan Tsvangirai alikuwa kibaraka wa Uingereza mwanzoni lakini kisha kuhamia kambi ya Amerika. Muingereza ana yakini kuwa watadumisha hali halisi lakini kilicho muhimu zaidi kwao ni kudandia hamasa za watu na hamu ya mabadiliko iso muelekeo na kuleta mabadiliko ya kisanii kupitia kumuunga mkono mmoja wa vibaraka wake kupanda ngazi ya utawala.

Bila ya kujali iwapo Grace Mugabe au Emmerson Mnangagwa ndiye atakaye panda ngazi ya utawala hilo kwao haliwashughulishi wala sio kipao mbele. Hivyo basi, yale yanayo shuhudiwa nchini Zimbabwe katika mgogoro uliopo sasa ni njama ya Uingereza kuwahadaa watu kuwa kuna mabadiliko ya kiutawala ilhali ukweli ni kuwa, yanayo endelea ni mabadiliko tu ya sura. Watu watakao panda ngazi ya utawala watadumisha mfumo ule ule wa kirasilimali na nidhamu zake ovu ikiwemo demokrasia na nidhamu ya kijamii na kiuchumi itakayo endelea kufuja mali ya umma na kuongeza zaidi viwango vya ufisadi wa kijamii na kiuchumi.



Email: uqab@hizb.or.ke